**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI**

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na.MMC/A40/29/VOL.IV/11** Tarehe: 15/11/2025

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Manispaa ya Moshi anawatangazia Watanzania wenye sifa kuomba nafasi za kazi tano (5) katika Manispaa hii baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mchanganuo ufuatao:-

### 1.0. MWANDISHI MWENDESHA OFISI DARAJA LA II – NAFASI 5

#### 1.1 KAZI NA MAJUKUMU

i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida na siri;
ii. Kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa;
iii. Kutunza taarifa na kumbukumbu za matukio, miadi, wageni,tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine;
iv. Kutafuta majalada na nyaraka zinazohitajika katika utekelezaji wa majukumu ya kazi;
v. Kupokea majalada na kusambaza kwa maofisa walio katika Idara/ Kitengo/ Sehemu husika;
vi. Kukusanya, kutunza na kuyarejesha majalada na nyaraka sehemu zinazohusika;
vii. Kupanga dondoo na kufanya maandalizi ya Vikao mbalimbali;
viii. Kuandaa orodha ya mahitaji ya vifaa vya Ofisi na
ix. Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

**1.2 SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa Wahitimu wa kidato cha Nne au sita ( Form IV / VI) mwenye Stashahada ya Uhazili au Cheti cha NTA level 6 ya Uhazili. Aidha awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kingereza maneno 100 kwa dakika moja na kupata program za Komputa za Ofisi kama Word, Excel, PowerPoint, E-mail na Publisher kutoka Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

**1.3 NGAZI YA MSHAHARA TGS C**

**2.0 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI**

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye Umri kati ya miaka 18 hadi 45
ii. Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye Mfumo wa kuombea ajira ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
iii. Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (***Detail Curriculum Vitae)*** yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na anuani ya barua pepe (E- mail Address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika;
iv. Maombi yote yaambatanishwe na nakala ya vyeti vya Elimu na Taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/ Wakili ambavyo ni vyeti vya kidato cha Nne au Sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika **Diploma/ Certificates, - Cheti cha Mitihani ya Kidato cha IV, VI, Computer Certificate, Vyeti vya Kitaaluma (Progfessional Certificate from Respective Boards).**
v. Testimonial “Provisional Result” Statement of Result “ hati za matokeo ya kidato cha nne au cha sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAZITAKUBALIWA.**
vi. Waombaji wote waliosoma nje ya Nchi wahakikishe kuwa vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika **(TCU, NECTA na NACTE)**.
vii. Waombaji waliostafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

viii. Waombaji wa kazi ambao tayari ni Waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na. **CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.**

ix. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika kuchukuliwa hatua za kisheria.

x. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **28/11/2025.**

xi. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:-

**Mkurugenzi wa Manispaa,**
**Halmashauri ya Manispaa ya Moshi,**
**S.L.P 318,**
**MOSHI-KILIMANJARO**

xii. Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa Kielekroniki wa Ajira **(Recruitment Portal)** kupitia anuani ifuatayo: https://portal.ajira.go.tz (Anwani hii pia inapatikana kwenyeTovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa "Recruitment Portal").

xiii. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu uliowasilishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA**.

Tangazo hili limetolewa na.

Mwajuma A. Nasombe
**MKURUGENZI**
**HALMASHAURI YA MANISPAA MOSHI**

Ukumbi wa Manispaa, S.L.P 318, MOSHI, KILIMANJARO. Simu: +255-027-2752344, +255-027-2754371/4, Nukushi: +255-027-2752906, Barua pepe md@moshimc.go.tz, Tovuti: www.moshimc.go.tz